BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU (HAKI NA FURSA) NAM. 9 YA MWAKA 2006 NA KUWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA WATU WENYE ULEMAVU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuanza kuwasilisha Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenye wingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha leo hii kutekeleza majukumu yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutujaalia amani na upendo, busara na hekima, pamoja na kutuzidishia neema zake zote ambazo ni muhimu sana katika maisha yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Watu wenye Ulemavu (Haki na Fursa) Nam. 9 ya Mwaka 2006 na Kuweka Masharti Yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Tunamuomba

Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; Mheshimiwa Harusi Said Suleiman kwa mashirikiano yake makubwa aliyotupatia Kamati hii wakati wa kuupitia Mswada huu lakini pia, nje ya Mswada huu amekuwa akitupa mashirkiano makubwa sana katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wa wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wao Dr. Omar Dadi Shajak kwa kusimamia vyema na kurekebisha Sheria hii ambayo itazidi kuweka usawa kwa Watu wenye Ulemavu pamoja na kutetea na kulinda haki na fursa zao katika jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa niwashukuru wadau wote wa Mswada huu ambao wameipitia kwa nafasi zao lakini pia wadau ambao walifika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ya kujenga na kuiwezesha Kamati kupata upeo mpana zaidi katika Masuala ya Watu Wenye Ulemavu hapa Zanzibar na Ulimwenguni kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, pongezi za pekee ziende kwa wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zao kubwa walizozionyesha katika kuwapatia wajumbe maarifa kuhusu mswada huu na kuwaelekeza mambo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika**, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa madhumuni ya Mswada huu ni kufuta Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa), Nam. 9 ya Mwaka 2006 na Kuweka Masharti Yanayohusiana na Watu Wenye Ulemavu na Mambo Mengine Yanayohusiana na ulemavu

ili kulinda na kuendeleza haki, maisha, maendeleo endelevu na jumuishi pamoja na kufikia kuwa na jamii jumuishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu imejitahidi kutumia uwezo wake wa kitaalamu, hekima na busara ili kuhakikisha Mswada huu umekuwa bora na wenye tija kwa walengwa ambao kwa muda mrefu jamii imekuwa ikiwafanyia mambo ambayo yanakinzana na mazingira ya kawaida kwa binadamu.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii itaeleza kwa ufupi sana baadhi tu ya Maoni ya Marekebisho ya Mswada huu kwani maelezo kamili yamewekwa kwenye waraka ambao tayari wajumbe wameshapatiwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi na uweze kufahamika na kila mmoja miongoni mwetu kwa lugha nyepesi na lenye kueleweka, Kamati yangu inashauri kufanya marekebisho jina refu la Mswada huu ili liweze kusomeka kama ifuatavyo:

"MSWADA WA SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA WATU WENYE ULEMAVU (HAKI NA FURSA) NAM. 9 YA MWAKA 2006 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI YANAYOHUSIANA NA WATU WENYE ULEMAVU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO".

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati yangu inapendekeza kufanywa marekebisho ya Kifungu cha 16(2) cha mswada huu kwa kufutwa maneno "**Baraza la Wilaya"** na kuwekwa badala yake maneno **"Baraza la Watu Wenye Ulemavu la Wilaya".** Aidha, marekebisho haya yafanyike kila yanapojitokeza katika

mswada huu ili kutofautisha Baraza hili la Watu wenye Ulemavu la Wilaya pamoja na Mabaraza mengine ambayo yanaanzishwa siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika,** katika Sehemu ya Nne ya Mswada huu ambayo inahusiana na haki na fursa, ufikiaji, wajibu wa haki za Watu Wenye Ulemavu na kuondoa ubaguzi na udhalilishaji katika jamii. Kamati inatumia nafasi kuishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuthamini na kuwezesha watu wenye ulemavu Zanzibar kwa kulinda na kusimamia haki zao za mawasiliano katika wakati huu ambao mawasiliano imekuwa nyenzo muhimu sana katika maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati yangu inashauri katika Kifungu cha 28 (1) kurekebishwa kwa kuingiza aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

**"haki ya kupata habari na mawasiliano kwa kuzingatia hali ya ulemavu".**

Aidha, itakuwa vyema kama aya hizi zikiwekwa katika mpangilio ulio sawa ili kwenda sambamba na mantiki iliyokusudiwa katika kifungu hiki. Kamati pia inaiomba Serikali kuwa na utaratibu wa haraka wa kuridhia Maazimio ya Kimataifa juu ya mambo na shughuli za Watu Wenye Ulemavu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha hotuba hii fupi kabisa kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati

imepata mafunzo ya kutosha juu ya Mswada huu ili kuufanya uwe bora na wenye kuleta maslahi kwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itawasaidia Watu Wenye Ulemavu kwa kuwapatia haki na fursa zao kama ilivyo kwa makundi mengine yaliyopo katika jamii yetu.

**Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha**.

Ahsante,

……………………………

(*Machano Othman Said*)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**